## AckySHINE.com

# Kwa nini watu wanakunywa pombe?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Unywaji wa pombe ni sehemu ya utamaduni wa Tanzania na nchi nyinginezo duniani.

Watu hupendelea kunywa pombe katika sherehe za kidini, kijamii, nyumbani na vilabuni. Wanakunywa pombe ili kujiburudisha, lakini pia kuongeza ujasiri, kuondoa aibu au kusahau matatizo yao kwa kipindi fulani au kwa muda mfupi.

Vijana wengi, hasa wavulana, hudhani kwamba kunywa pombe ni ishara ya kujionyesha kuwa wamekuwa watu wazima. Kimsingi, unywaji pombe kidogo hukubalika kijamii na hauna madhara, lakini ulevi wa kupindukia ni hatari na huweza kusababisha vifo na haukubaliki katika jamii zetu kwa sababu hudhoofisha na kufanya watu kusahau majukumu yao, hupunguza heshima na afya njema.